# NAFASI ZA KAZI (17)

## MTIBWA SUGAR ESTATES LIMITED

*"Mtibwa Sugar kumenoga, njooni tuungane"*

**18 JULAI 2025**

### 1. Utangulizi

Mtibwa Sugar Estates Limited ni kampuni inayojishughulisha na uzalishaji wa miwa na utengenezaji wa sukari katika eneo la Mtibwa – Turiani – Mvomero – Morogoro – Tanzania.

Sifa mojawapo ya Mtibwa Sugar ni kufanya kazi kwa ushirikiano (teamwork). Mtu yeyote anayefanikiwa kuwa miongoni mwa wafanyakazi wa Mtibwa Sugar anakuwa mwanafamilia wa Mtibwa Sugar na hatajuta kwa maamuzi yake hayo kwani atapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wafanyakazi wenzake na Utawala kwa ujumla. Pia Mtibwa Sugar inajali kukuza vipaji na fani mbalimbali kwa wafanyakazi wote.

### 2. Nafasi za kazi za kuomba

**i. Mwanasheria (Legal Officer) nafasi 1**

(a) Awe Wakili
(b) Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 5
(c) Awe Mtanzania
(d) Umri usiozidi miaka 45

**ii. Mkaguzi wa ndani (Internal Auditor) nafasi 1**

(a) Awe na shahada ya uhasibu
(b) CPA ni lazima.
(c) Uzoefu wa kazi za ukaguzi wa ndani usiopungua miaka 5
(d) Awe Mtanzania
(e) Umri usiozidi miaka 45

**iii. Afisa Mazingira, Afya na Usalama mahala pa kazi (EHS Officer) nafasi 5**

(a) Shahada ya kwanza ya Uhandisi, mazingira, afya, usalama mahala pa kazi au inayoendana.
(b) Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 2
(c) Awe Mtanzania
(d) Umri usiozidi miaka 45



CamScanner

iv. **Msimamizi wa Ubora (Quality Supervisor) nafasi 1**

(a) Shahada ya usalama wa chakula au inayoendana nayo.
(b) Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 3
(c) Awe Mtanzania
(d) Umri usiozidi miaka 45

v. **Meneja wa Ubora, Usalama, Afya na Mazingira (SHEQ Manager) nafasi 1**

(a) Shahada ya kwanza ya Uhandisi, mazingira, afya, usalama mahala pa kazi au inayoendana.
(b) Uzoefu usiopungua miaka 4 (minne) katika ngazi ya Meneja katika eneo husika.
(c) Awe Mtanzania
(d) Umri usiozidi miaka 45

vi. **Afisa Tabibu (Clinical Officer) nafasi 2**

(a) Awe amesajiliwa na awe na leseni hai inayomruhusu kufanya kazi ya Afisa tabibu
(b) Awe na uzoefu usiopungua miaka 2
(c) Awe Mtanzania
(d) Umri usiozidi miaka 45

vii. **Daktari (Medical Doctor) nafasi 1**

(a) Awe amesajiliwa
(b) Awe na leseni hai
(c) Uzoefu kazini usiopungua miaka 2
(d) Awe Mtanzania
(e) Umri usiozidi miaka 45

viii. **Afisa kumbukumbu Mwandamizi (Senior Records Officer) nafasi 1**

(a) Awe na Shahada katika fani ya kumbukumbu
(b) Awe na uzoefu katika usimamizi wa kumbukumbu kama Mkuu wa Kitengo kwa muda usiopungua miaka 5
(c) Awe na umri usiozidi miaka 45
(d) Awe Mtanzania

ix. **Mtawala wa Hospitali (Hospital administrator) nafasi 1**

(a) Awe na Shahada ya Usimamizi wa mifumo ya Afya.
(b) Awe na uzoefu wa kazi katika usimamizi wa Hospitali usiopungua miaka 5.
(c) Awe na umri usiozidi miaka 45
(d) Awe Mtanzania



CamScanner

x. **Mtaalamu wa matengenezo ya vifaa au mashine kiwandani kulingana na hali halisi ya vifaa au mashine - Condition Based Maintenance Technician (CBM) nafasi 1**
(a) Stashahada katika Uhandisi wa Mitambo au umeme
(b) Awe na uzoefu usiopungua miaka 2 katika viwanda vikubwa.
(c) Awe na umri usiozidi miaka 45
(d) Awe Mtanzaniag

xi. **Mwanafunzi mhitimu katika uhandisi wa vipimo (Graduate Trainee in Instrumentation Engineering) nafasi 2**
(a) Shahada ya uhandisi wa umeme na elektroniki
(b) Awe na umri usiozidi miaka 35
(c) Awe Mtanzania

### 3. Namna ya kutuma maombi na Viambatanishi

Maombi yote yatumwe kwa barua pepe Hr@mtibwa-sugar.co.tz au yapelekwe katika ofisi za HR - MTIBWA au yatumwe kwa njia ya POSTA.

Meneja Rasilimali Watu na Utawala, S.L.P 42, Mtibwa, Morogoro.

### 4. Viambatanishi

Mwombaji aambatanishe wasifu (CV), picha yake ya hivi karibuni (passport size), leseni ya fani husika, vyeti, TIN, NIDA au kitambulisho cha kura na cheti cha kuzaliwa.

### 5. Angalizo

(a) Mwombaji awe tayari kufanya kazi na kuishi Mtibwa
(b) Mwombaji asiwe na rekodi ya kukutwa na hatia ya jinai mahakamani

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31/07/2025.**

Tunatanguliza shukrani

MTIBWA SUGAR ESTATES LTD
10 JUL 2025
P.O. Box 42, MTIBWA

Shani Christoms Mligo

Mkuu wa Idara

Rasilimali Watu na Utawala



CamScanner